# KUHAMISHWA KWA MFUNGWA AMBAYE HAJAHUKUMIWA KWENDA KWA HOSPITALI (NA VIZUIZI AU BILA VIZUIZI)

(Sehemu ya 48 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa | |
| 2. Jina la mtu anayesimamia utunzaji wako (“daktari wako anayewajibika”) | |
| 3. Jina la hospitali na wadi | |
| 4. Tarehe ya agizo la kuhamishwa kwako | |
| 5. Agizo la kizuizi limewekwa? | Ndio/ Hapana |

## Je! ni kwanini niko hospitalini?

Umehamishwa kuja katika hospitali hii kwa sababu Katibu wa Haki wa Jimbo ameshauriwa na madaktari wawili kuwa unayo shida ya akili na kuwa unahitaji kuwa katika hospitali kwa matibabu ya kiakili.

Katibu wa Haki wa Jimbo ametoa “agizo la uhamisho” chini ya sehemu ya 48 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983 ambayo inaruhusu mfungwa ambaye hajahukumiwa kuhamishwa kwenda kwa hospitali.

Katibu wa Jimbo pia anawezakuwa ametoa agizo la kizuizi chini ya sehemu ya 49 ya Sheria ya Afya ya Akili.

## Je! agizo la kizuizi ni nini?

Ikiwa umepewa agizo la kizuizi, inamaanisha kuwa hauwezi kuruhusiwa kutoka katika hospitali isipokuwa kama Katibu wa Haki wa Jimbo aseme kuwa unaweza kutoka. Katika hali hii, kuruhusiwa kwako kutoka kunaweza kutegemea masharti fulani ambayo yatafafanuliwa kwako karibu na wakati huo. Ukiwa hospitalini, mtu anayesimamia utunzaji wako (daktari wako anayewajibika) lazima apate makubaliano ya Katibu wa Haki wa Jimbo kabla uweze kuenda kwa likizo fupi au utumwe katika hospitali nyingine.

## Je! nitakuwa hapa kwa muda gani?

Utawekwa katika hospitali hadi agizo lako la kuhamishwa liishe.

Ikiwa umehamishwa kuja hapa **baada ya kuzuiliwa na Korti ya Hakimu:**

> Utawekwa hospitalini hadi kipindi chako cha kuzuiliwa kiishe, isipokuwa ukitumwa kwa Korti ya Utawala kushtakiwa *au* uzuiliwe tena na Korti ya Hakimu' (ambapo katika hali hiyo utakaa hospitalini). Korti ya Hakimu pia inaweza kuamuru agizo la kuhamishwa liishe ikiwa daktari wako anayewajibika amesema kuwa hauhitaji tena matibabu ya shida ya akili katika hospitali. Basi utarudi gerezani, isipokuwa korti iamue kukuwachilia kwa dhamana.

Ikiwa umehamishwa kuja hapa **kama mfungwa wa serikali au chini ya sheria za umamiaji**:

> utawekwa kwenye hospitali hadi tarehe ambayo utakuwa umewachiliwa kutoka gerezani au umetolewa kutoka kwenye kituo cha kuzuiliwa, isipokuwa daktari wako anayewajibika aseme kuwa hauitaji tena matibabu. Ikiwa umepewa agizo la kuzuiliwa na daktari wako aseme kuwa hauitaji tena matibabu, utarudishwa gerezani au kwenye kituo cha kuzuiliwa.

**Katika hali zingine:**

> utawekwa hospitalini hadi daktari wako anayewajibika aseme kuwa hauitaji tena matibabu au hadi kesi yako iwe imeamuliwa na korti. Ikiwa daktari wako anayewajibika amesema kuwa hauitaji tena matibabu utarudishwa gerezani, isipokuwa korti iamue kukuwachilia kwa dhamana.

## Je! ninaweza kuwekwa katika hospitali baada ya agizo la kuhamishwa kuisha?

Inawezekana kuwa utawekwa katika hospitali chini ya sehemu tofauti ya Sheria ya Afya ya Akili ikiwa unahitaji matibabu baada ya agizo lako la kuhamishwa kuisha. Ikiwa hivyo, utapewa kijikaratasi kingine kufafanua haya.

## Je! ni nini kitakachofanyika ikiwa ninapaswa kurudi kortini?

Ikiwa uko katika kizuizi na hujashtakiwa, unaweza hitajika kurudi kortini. Korti itaangalia kesi yako na inawezatoa amri ya hospitali chini ya sehemu ya 37 au Sheria ya Afya ya Akili ikisema unapaswa kukaa katika hospitali, au inwezatoa hukumu tofauti. Korti inaweza tu kutoa amri ya hospitali ikiwa madakatari wawili waseme kuwa una shida ya akili na kuwa unahitaji kutibiwa chini ya Sheria ya Afya ya Akili.

## Je! ninaweza kuomba rufaa?

Hauwezi kuomba rufaa kinyume na uamuzi wa Katibu wa Jimbo wa Haki kukuhamisha kwenda kwa hospitali, au kinyume na kizuizi na korti ya hakimu.

Lakini kuna watu unaweza kuuliza wakuruhusu utoke hospitalini.

Ikiwa hujapewa agizo la kuzuiliwa, unaweza kuuliza Wasimamizi wa Hospitali wakuruhusu utoke hospitalini. Unaweza kufanya hivi wakati wowote. Wasimamizi wa shule ni kamati maalum ya watu iliyowekwa kwenye hospitali kuamua ikiwa watu wanapaswa kewekwa hospitalini. Wasimamizi wa Hospitali wanaweza kutaka kuzungumza nawe kabla ya kuamua kama watakuruhusu uende. Ikiwa unataka kufanya hivi, unaweza kuwaandikia kwa:

| |
|---|
| |

Au unaweza kuuliza mfanyikazi kukusaidia kuwasiliana na Wasimamizi wa Hospitali.

Hata ikiwa umepewa au hujapewa agizo la kuzuiliwa, unaweza kuliza Mahakama iseme kuwa haupaswi kuwekwa hospitalini.

## Mahakama ni nini na nini hufanyika?

Mahakama ni Jopo la kujitegemea ambalo linaweza kuamua kama unapaswa kuruhusiwa kutoka hospitalini. Itafanya mkutano na wewe na wafanyikazi  wanaokujua kutoka kwa hospitali hiyo. Mkutano huu unaitwa “usikilizaji”. Unaweza kumuuliza mtu mwingine aje kwenye usikilizaji huo kukusaidia. Ikiwa unataka Kabla ya usikilizaji, washiriki wa Mahakama watasoma ripoti kukuhusu na utunzaji wako kutoka kwa hospitali. Mmoja wa washiriki wa mahakama pia watakuja kuzungumza nawe.

## Je! ni lini ninaweza kutuma ombi kwa mahakama?

Unaweza kutuma ombi kwenye Mahakama mara moja wakati wowote katika miezi sita ya kwanza uliyopewa agizo la kuhamishwa.

Kisha unaweza tuma ombi tena wakati wa miezi sita inayofuata kisha mara moja kila mwaka uliowekwa kwenye hospitali baada ya hapo.

Ikiwa haujapewa agizo la kuzuiliwa, jamaa wako wa karibu zaidi anaweza kuomba Mahakama mara moja wakaiti wa pili wa miezi sita baada ya agizo la uhamisho wako na mara moja kila mwaka baadaye. Kijikaratasi hiki kinafafanua zaidi jamaa wako wa karibu zaidi ni nani.

Ikiwa unataka kuomba kwa Mahakama unaweza kuandika kwa:

The Tribunals Service
PO BOX 8793
5th Floor
Leicester
LE1 8BN Simu 0300 123 2201

Unaweza kumuuliza wakili aandikie Mahakama kwa usaidizi wako katika usikilizaji. Hospitali na Jamii ya Sheria wana orodha ya wakili ambao wana utaalam katika haya. Hautahitajika kulipa kwa usaidizi wa wakili kwa haya. Ni bure chini ya Mpango wa Usaidizi wa Kisheria.

## Je! ni nini kitakachofanyika ikwa hamakama itasema sipaswi kuwekwa katika hospitali?

Ikiwa mahakama imesema kuwa haupaswi kuwekwa katika hospitali, inaweza kumaanisha urudishwe gerezani au kituo cha kuzuiliwa, isipokuwa Mahakama imependekeza kuwa ukae katika hospitali.

## Je! nitapewa matibabu gani?

Daktari wako anayewajibika na wafanyikazi wengine watazungumza nawe kuhusu matibabu yoyote unayoweza kuhitaji kwa shida yako ya akili. Katika hali nyingi utalazimika kukubali ushauri wao.

Baada ya miezi tatu, kuna sheria maalum kuhusu dawa zozote au madawa unayopewa kwa shida yako ya akili. Ikiwa hautaki dawa au madawa hayo, au wewe ni mgonjwa sana kusema kama unayataka, daktari ambaye hatoki katika hospitali hii atakutembelea. Daktari huyu wa kujitegemea atazungumza nawe na wafanyikazi katika hospitali wanaokujua. Daktari wa kujitegemea ataamua ni dawa au madawa yapi unaweza kupewa. Isipokuwa ni dharura, hii tu ndio dawa au madawa unayoweza kupewa bila makubaliano yako.

Daktari huyu wa kujitegemea anaitwa SOAD (Daktari wa Maoni ya pili aliyewekwa) (Second Opinion Appointed Doctor) ni ameteuliwa naTume inayojitegemea ambayo inaangalia jinsi Sheria ya Afya ya Akili inatumika.

Kuna sheria tofauti za matibabu fulani maalum, kama Tiba ya Kuikisa kupitia stima (ETC). Ikiwa wafanyikazi wanafikiria unahitaji moja ya matibabu haya maalum, sheria zitafafanuliwa kwako ma utapewa kijikaratasi kingine.

## Kumjulisha jamaa wako wa karibu zaidi

Ikiwa haujapewa agizo la kuzuiliwa, nakala au kijikaratasi hiki kitapewa mtu ambaye Sheria ya Afya ya Akili imesema ndiye jamaa wako wa karibu zaidi.

Kuna orodha ya watu katika Sheria ya Afya ya Akili ambao wanachukuliwa kama jama. Kwa kawaida, mtu anayekuja juu kabisa kwenye orodha ndiye jamaa wako wa karibu zaidi. Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kukupa kijikaratasi kinachoeleza haya na ni haki gani  jamaa wako wa karibu zaidi anazo kuhusiana na utunzaji na matibabu yako.

Katika hali yako, tumeambiwa kuwa jamaa wako wa karibu zaidi ni:

| |
|---|
| |

Ikiwa hautaki mtu huyu kupata nakala ya kijikaratasi hiki, tafadhali ambia muuguzi wako au mfanyikazi mwingine.

## Kubadilisha jamaa wako wa karibu zaidi

Ikiwa haufikirii kuwa mtu huyu anafaa kuwa jamaa wako wa karibu zaidi, unawezaomba mtu mwingine achukuliwe kama jamaa wako wa karibu zaidi badala yeke kwenye Korti ya Mkoa. Wafanyikazi wa hospitali wanawezakupa kijikaratasi kinachofafanua haya.

## Barua Zako

Barua zote ulizotumiwa utapewa. Unaweza kutuma barua kwa mtu yeyote isipokuwa mtu aliyesema hataki kupokea barua kutoka kwako. Barua za watu hao zinaweza kuzuiliwa na wafanyikazi wa hospitali.

## Kanuni za Kufanya kazi

Kuna Kanuni za Kufanya kazi zinazotoa ushauri kwa wafanyikazi hospitalini kuhusu Sheria ya Afya ya Akili na kutibu watu walio na shida ya akili. Wafanyikazi wanapaswa kuzingatia Kanuni inasema nini wakati wanapofanya uamuzi kuhusu utunzaji wako. Unaweza kuuliza nakala ya Kanuni, ikiwa unataka.

## Ninapaswa kulalamika aje?

Ikiwa unataka kulalamika kuhusu jambo lolote linalohusiana na utunzaji wako na matibabu katika hospitali tafadhali ongea na mfanyikazi. Hii inaweza kusaidia kutatua swala hilo. Wanaweza kupa habari kuhusu utaratibu wa malalamishi ya hospitali, ambayo unaweza kutumia kujaribu kutatua malalamishi yako kupitia jambo linaitwa suluhisho za kawaida. Wanaweza pia kukuambia kuhusu watu wengine wowote ambao wanaweza kukusadia kulalamika.

Ikiwa hauhisi kuwa utaratibu wa malalamishi ya hospitali unweza kukusaidia, unaweza kulalamika kwa Tume ya Kujitegemea. Tume hiyo huchunguza jinsi Sheria ya Afya ya Akili inatumika, kuhakikisha inatumiwa vyema na kuwa wagonjwa wanatunzwa vyema wakiwa

hospitalini. Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kukupa kijikaratasi kinachofafanua jinsi ya kuwasiliana na Tume.

## Usaidizi na habari zaidi

Ikiwa kuna jambo lolote ambalo hauelewi kuhusu utunzaji wako na matibabu yako, wafanyikazi watajaribu kukusaidia. Tafadhali uliza mfanyikazi kukufafanulia ikiwa kuna jambo lolote katika kijikaratasi hiki ambalo hauelewi au ikiwa una maswali mengine ambayo kijikaratasi hiki hakijajibu.

Tafadhali uliza nakala nyingine ya kijikaratasi hiki ukitaka kumpa mtu mwingine.